

YAH: TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inawakaribisha watoa huduma na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki na kutembelea Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (41 DITF) yanayotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 28 Juni hadi 8 Julai, 2017 katika Uwanja wa Maonesho ya Biashara wa Mwalimu J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Kauli Mbiu ya Maonesho haya ni **UKUZAJI WA BIASHARA KWA MAENDELEO YA VIWANDA**. Kauli Mbiu hii inalenga kutumia Maonesho haya kama jukwaa la kutangaza biashara na huduma mbalimbali kwa ajili ya ukuzaji wa Sekta ya Viwanda ikizingatiwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inaweka mkazo mkubwa katika kuendeleza uchumi wa viwanda hapa nchini.

Kupitia Maonesho haya, Washiriki watatangaza huduma na bidhaa wanazozalisha ili kupata masoko endelevu ya nje na ndani ya nchi, kujenga mtandao kibiashara na kupata teknolojia za kisasa na kujifunza mbinu mpya za kuendeleza biashara zao.

Pia, Maonesho haya, yatawapa fursa wenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kukutana na wanunuzi wa bidhaa zao na kampeni maalum ya kuhamasisha Wananchi kupenda bidhaa zinazozalishwa hapa nchini itafanyika.

Maonesho haya yamekuwa yakipata umaarufu mwaka hadi mwaka na kuongeza idadi ya waoneshaji na watembeleaji kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi nyingine za Afrika, Asia, Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani

Ili kushiriki Maonesho haya unaweza kupakua Fomu kupitia tovuti ya Taasisi ambayo ni www.tantrade.or.tz au unaweza tembelea ofisi za Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) zilizopo katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam ambao ni waratibu wa Maonesho. Kwa maelezo zaidi waweza kutupigia simu kupitia namba +255 786 232386 au barua pepe info@tantrade.or.tz

Wote Mnakaribishwa.

Imetolewa na:



Theresa Chilambo

MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO WA UMMA NA MAWASILIANO

30 Machi, 2017